DIBAJI

Mamlaka za Serikali za Mitaa zilianzishwa ili kutekeleza na kukidhi matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kwa lengo la kuwapa Wananchi uwezo wa kujiamualia masuala yao ikiwemo uchumi na kuinua hali za maisha . Katika Ibara za 145 na 146 ya Katiba imetamkwa wazi kuwepo kwa vyombo vya wananchi ambavyo vitaanda mazingira wezeshi ya kupeleka madaraka kwa wananchi na kutoa fursa kwa wananchi kushiriki katika kubuni, kupanga, kutekeleza na kusimamia mipango ya kijamii na kiuchumi.

Sera ya ugatuaji madaraka ya mwaka 1998 imesisitiza kuongeza uwezo wa kifedha kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kujiendesha zenyewe.Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 imeainisha vyanzo vya mapato kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo Mikopo ni miongoni mwa vyanzo hizo.Pamoja na kuwepo kwa Sheria Sura 290,Sheria Na. 30 ya mwaka 1974 na marekebisho pia inasimamia Mikopo kwa Taasisi za Umma zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Pamoja na kuwepo kwa Sera na Sheria hizi, bado kumekuwepo na changamoto mbalimbali ikiwemo kutokuwa na fedha za kutosha na mifumo dhaifu ya udhibiti wa rasilimali zilizopo. Hali hii imesababisha Halmashauri kushindwa kujiendesha kwa ufanisi, kujenga miundombinu bora na ya kisasa na kutoa huduma bora kwa wananchi kama ilivyokusudiwa.

Ili kukabiliana na changamoto hizo na kuziongezea Mamlaka za Serikali za Mitaa uwezo wa kifedha kwa njia ya mikopo kutoka vyanzo mbalimbali, Ofisi yangu imepitia na kuandaa mwongozo ambao unapaswa kuzingatiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zote zinazotarajiwa kukopa. Mwongozo huu umeandaliwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Kisekta katika usimamizi wa fedha na Mikopo.

Ni matarajio yangu kuwa, kuanzia tarehe ya matumizi ya mwongozo huu, Halmashauri zote zitazingatia na kujiridhisha kuwa maombi yao ya mikopo yamekidhi matakwa ya mwongozo huu kabla ya kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa.

Hawa A. Ghasia (Mb.)
WAZIRI WA NCHI
OWM - TAMISEMI

Y A L I Y O M O

SEHEMU YA KWANZA

Ukurasa

1.0 Utangulizi……..…….... 2

1.1 Taratibu za Mikopo, Sheria zinazosimamia mikopo na jinsi muundo wa Mwongozo utakavyokuwa…..……..…… 2

SEHEMU YA PILI

2.0 Masuala muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandaa nyaraka za maombi ya mkopo katika Mamlaka ya Merikali za Mitaa……..…… 7

SEHEMU YA TATU

3.0 Maelekezo ya namna ya kusimamia miradi mbalimbali inayotokana na fedha za mikopo …….. 12

4.0 Hitimisho ……...… 16

Kiambatisho……..……....…… 17

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI:

1.1 Taratibu za Mikopo, Sheria zinazosimamia mikopo na jinsi muundo wa Mwongozo utakavyokuwa:

Serikali za Mitaa ni vyombo vya wananchi ambavyo vinaundwa na kuendeshwa kwa mujibu wa Sheria Sura 287 na 288. Majukumu ya Serikali za Mitaa yameainishwa katika Sheria zilizotajwa ambapo wajibu na majukumu hayo yamezingatia mazingira ya Kijiografia, Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinajumuisha Serikali za Vijiji, Mamlaka za Miji Midogo na Halmashauri. Halmashauri zimepangwa katika makundi mawili ambayo ni Halmashauri za Miji na Halmashauri za Wilaya. Msingi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni ushirikishwaji na uhusishwaji wa Wananchi katika maamuzi na usimamizi wa masuala ya maisha na maendeleo yao.

Baraza la Madiwani ndicho chombo chenye Mamlaka ya juu katika maamuzi yote yanahusu Halmashauri. Wajumbe wa Baraza la Madiwani wanatokana na wajumbe wa kuchaguliwa moja kwa moja na wananchi kutoka katika kila Kata zilizomo katika himaya ya Halmashauri pamoja na Wajumbe walioteuliwa na Vyama vya Siasa. Mwaka 1998 Serikali iliunda Sera ya Ugatuaji madaraka kwenda kwa Wananchi kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sera hii imetaja maeneo yanayo gatuliwa kuwa ni pamoja na masuala ya kisiasa, rasilimali watu na rasilimali fedha. Hatua hii inalenga kuongeza na kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika uendeshaji shughuli za Umma.

Miongoni mwa masuala ya msingi katika kuimarisha uhai na maendeleo na ukuaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kuwepo kwa mapato ya kutosha kwa ajili ya kulipia gharama za uendeshaji, utoaji huduma na uboreshaji

miundombinu.

Vyanzo vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa vimetajwa katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 vifungu vya 6, 7, 8, 9, 12, 13, 14 na 15. Vyanzo hivi vimegawanywa katika makundi ya vyanzo vya ndani vya Halmashauri, ruzuku kutoka Serikali Kuu, na mikopo. Mikopo imetajwa katika Kifungu cha 14 cha Sheria Sura 290, kadhalika ipo Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Na. 30 ya mwaka 1974 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2004) na Kanuni zake. Sheria hizi hazina budi kufanya kazi kwa pamoja.

Mwongozo huu haukusudii kuchukua nafasi ya Sheria mama ya mikopo (Sheria Na. 30 ya mwaka 1974), bali una dhamira ya kurahisisha matayarisho, uwasilishaji maombi, utekelezaji, tathmini na ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo. Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia Sheria ya Serikali ya Mikopo na Dhamana na pia

umezingatia Kanuni za Usimamizi wa Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 2009 *(Local Authorities Financial Memorandum, 2009)*. Mwongozo wa mikopo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa unalenga kutoa maelekezo ya hatua kwa hatua kuanzia maandalizi ya maombi ya mikopo, uwasilishaji, uhakiki, ufuatiliaji matumizi ya mikopo, marejesho na utoaji taarifa za mikopo. Mikopo inatarajiwa kugharamia miradi ya kiuchumi lakini pia miundombinu ya huduma za jamii kwa dhamana ya uwezo wa mapato ya vyanzo vya ndani vya mapato vya Halmashauri.

Mwongozo huu una sehemu kuu tatu, Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi juu ya masuala ya mikopo na unazungumzia juu ya sheria zinazosimamia mikopo na jinsi muundo wa mwongozo utakavyokuwa. Sehemu ya pili inahusu masuala muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandaa maombi ya mikopo na maelekezo ya namna ya kuandaa taarifa na nyaraka mbalimbali

za maombi ya mikopo, Sehemu ya tatu inahusu namna ya kusimamia miradi mbalimbali itakayotekelezwa kwa fedha za mikopo na maelekezo mahsusi ya namna ya kutayarisha taarifa za miradi mbalimbali inayotekelezwa kwa fedha za mikopo.

SEHEMU YA PILI

2.0 MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA WAKATI WA KUANDAA NYARAKA ZA MAOMBI YA MKOPO KATIKA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA

Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepewa Mamlaka ya Kisheria kukopa kutoka Taasisi za Fedha na Benki kwa mujibu wa Kifungu Na. 14(1), (2), (3) (4) na *14(5)* cha Sheria ya fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura Na. 290.

Mamlaka hizi zinaweza kukopa au kuingia ubia na Taasisi mbalimbali za kifedha baada ya kupata kibali kutoka kwa Waziri mwenye Dhamana na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, zinapaswa kuzingatia taratibu zote muhimu zinazohusu maandalizi na uwasilishaji maombi ya mikopo kwa kuzingatia na kutekeleza maelekezo yafuatayo:-

2.1 Mamlaka ambayo inakusudia kukopa inapaswa

kuzingatia taratibu zilizoainishwa kwenye Agizo Na. 51 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 (LAFM – 2009) inayoagiza kuwa; Halmashauri inayotaka kukopa lazima iwasilishe maombi kwenye Kamati ya Kudumu ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa ajili ya kujadiliwa na kukubaliwa na kuwasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani ili yaweze kupata kibali.

2.2 Maombi ya kukopa yaliyokubaliwa na kuidhinishwa na Vikao vya Kamati za Kudumu husika za Halmashauri yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Maombi hayo yaambatishwe na Kiziduo cha kumbukumbu za Mkutano wa Baraza la Madiwani na Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango uliopitisha maombi hayo. Muhtasari wa Vikao hivi uoneshe kwa uwazi majadiliano na maamuzi mahsusi yaliyofikiwa juu ya suala hili.

Maombi ya mkopo ni lazima yaoneshe Taasisi ya Fedha au Benki inayotoa mkopo, madhumuni ya mkopo huo, kiasi cha mkopo, masharti ya mkopo, kiwango cha riba, muda wa marejesho ya mkopo, taratibu za urejeshaji, na gharama nyinginezo. Maombi hayo yataje miradi itakayotekelezwa kutokana na kiasi cha fedha za mkopo husika.

2.3 Maombi yaambatishwe na andiko la mradi ili kujua uwezekano wa matarajio ya mafanikio ya miradi husika na yataje athari zitakazo tokea *(outcomes and impacts)* kwa jamii.

2.4 Maombi ya mkopo yaambatishe mchanganuo wa matarajio ya mapato ya mradi ya kila mwaka na namna marejesho yatakavyokuwa yanafanyika, maombi yaoneshe vyanzo vya mapato vitakavyotumika katika kulipa mkopo husika, na yaoneshe mtiririko wa makusanyo ya ndani ya Halmashauri kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Pia, Halmashauri ni lazima iwasilishe mpango na bajeti ya makusanyo ya ndani ya

mwaka wa uwasilishaji wa maombi hayo.

2.5 Maombi ya mkopo yaambatane na Taarifa za Mwisho za Hesabu za Halmashauri zilizokaguliwa *(Audited Financial Statements)* za miaka mitatu iliyopita.

2.6 Kiasi cha mkopo kinachoombwa kisiwe zaidi ya wastani wa makusanyo ya ndani ya Halmashauri ya miaka minne iliyopita pamoja na makadirio ya mwaka husika. Aidha gharama za mkopo pamoja na marejesho kwa mwaka husika wa fedha zisiwe zaidi ya asilimia 30 ya wastani wa makusanyo ya ndani.

2.7 Maombi yaoneshe mfumo wa usimamizi ulioandaliwa na Mamlaka husika katika kuhakikisha thamani ya fedha inazingatiwa katika matumizi ya fedha za mkopo.

2.8 Maombi ya Mikopo yote ya Halmashauri au Mamlaka za ngazi za msingi za Serikali za Mitaa ni lazima yawasilishwe kwa Katibu Tawala Mkoa ambaye atahakikisha kuwa taarifa zote zilizomo

kwenye maombi ni sahihi na kamili kabla ya maombi ya mkopo kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu, OWM-TAMISEMI.

2.9 OWM – TAMISEMI pamoja na Ofisi za Mikoa watafanya ufuatiliaji wa mikopo iliyopokelewa ili kuona kama mikopo hiyo inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na marejesho yanafanyika kwa wakati ili kuepuka riba na tozo za kuchelewa kurejesha na kuepusha mizigo kwa Wananchi.

2.10 Waziri mwenye Dhamana atatoa kibali cha kukopa kwa mujibu wa Sheria Sura 290 Kifungu 14.

2.11 Halmashauri ihakikishe kuwa mradi unaotekelezwa kama utahusu ujenzi, miliki ya ardhi husika inamilikiwa na Halmashauri, imepimwa na ina hati miliki ili kuepusha migogoro ya ardhi wakati wa utekelezaji wa mradi.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAELEKEZO YA NAMNA YA KUSIMAMIA MIRADI MBALIMBALI INAYOTOKANA NA FEDHA ZA MIKOPO:

3.1 Ni wajibu wa kila Mkurugenzi wa Halmashauri iliyokopa kuhakikisha mkopo unatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na taarifa inatolewa ndani ya kipindi kilichooneshwa katika mpango kazi wa mradi.

3.2 Ni wajibu wa kila Mkurugenzi wa Halmashauri iliyokopa kusimamia utekelezaji wa miradi yote inayotekelezwa kwa fedha za mikopo na kuhakikisha marejesho yanafanyika kwa wakati.

3.3 Bila kuathiri maelekezo ya Sheria nyingine Mkurugenzi lazima awasilishe kwenye vikao vya Kamati ya Fedha, na Uongozi na Mipango taarifa za fedha za mkopo zilizopokelewa, matumizi ya fedha za mikopo na kiasi cha fedha

kinachorejeshwa kwa kila kipindi kwa mujibu wa masharti ya Mkopo.

3.4 Taarifa za utekelezaji wa miradi ya fedha za mikopo pamoja na taarifa za fedha za mikopo ikiwemo kiasi cha fedha kinachorejeshwa kila kipindi (mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka) ziwasilishwe kwa Katibu Tawala Mkoa zikiambatishwa na viziduo vya kumbukumbu za vikao vya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango. Katibu Tawala Mkoa baada ya kuzihakiki na kutoa maoni taarifa hizo ataziwasilisha kwa Katibu Mkuu OWM-TAMISEMI ambapo zitachambuliwa na zitaunganishwa kwa matumizi ya Ofisi na Wadau mbalimbali.

3.5 Ni wajibu wa kila Mkurugenzi kuhakikisha mikopo imeoneshwa katika mpango na bajeti ya mwaka husika kabla ya kuwasilisha maombi haya kwa Waziri mwenye Dhamana.

3.6 Wakurugenzi wanaopata uhamisho kutoka kituo

kimoja cha kazi kwenda kituo kingine ni lazima wakabidhi rasmi mpango wa malipo ya sehemu ya mikopo ambayo haijarejeshwa. Makabidhiano yaoneshe kumbukumbu na nyaraka zote za msingi katika kuthibitisha uwepo wa deni na thamani ya deni lenyewe. Taarifa ya Makabidhiano ipelekwe kwa Katibu Tawala Mkoa ambaye baada ya kujiridhisha ataiwasilisha kwa Katibu Mkuu OWM - TAMISEMI.

3.7 Ni wajibu wa kila Mkurugenzi kuteua Meneja wa mradi iwapo makubaliano na wakopeshaji au wabia hawakuzungumzia suala hilo ili kuimarisha uwajibikaji, ufuatiliaji, utunzaji wa kumbukumbu na utoaji wa taarifa wakati wote wa utekelezaji wa mradi.

3.8 Katibu Tawala wa Mkoa ambaye Halmashauri yake inaomba mkopo atahakiki maombi hayo na kutoa maoni yake kwa Katibu Mkuu OWM – TAMISEMI kama mkopo huo ni muhimu na una tija kwa Halmashauri husika.

3.9 Kila Katibu Tawala wa Mkoa anapaswa kuandaa utaratibu madhubuti wa ufuatiliaji wa Mikopo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mkoa una wajibu wa kukagua usimamizi wa matumizi ya fedha za mikopo, mpango na marejesho ya fedha za mikopo ya Halmashauri. Katibu Tawala Mkoa ataandaa taarifa ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ikiwemo miradi ya fedha za mikopo ambayo ataiwasilisha kwa Katibu Mkuu OWM - TAMISEMI. Taarifa hiyo ya ufuatiliaji iwasilishwe OWM – TAMISEMI kila baada ya miezi mitatu ambapo itaunganishwa na kupata taarifa ya nchi nzima. (*Fomati ya uwasilishaji wa taarifa ya Halmashauri zilizoomba mikopo - tafadhali angalia Kiambatisho A).*

4.0 HITIMISHO:

Ni wajibu wa kila Katibu Tawala wa Mkoa kuhakikisha kuwa anasimamia ufuatiliaji na tathmini ya usimamizi na utelekelezaji wa miradi na makubaliano ya mkopo. Mkoa hauna budi kutoa msaada wa ushauri katika masuala ya mikopo na usimamizi wa miradi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mpango madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini utaziepusha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuingia katika madeni yasiyo ya lazima na kuhakikisha vipengele vyote katika mwongozo huu vinafuatwa ipasavyo.

Mwongozo huu ni utaratibu rasmi wa kuzingatia katika kutayarisha maombi, uwasilishaji, uhakiki, ufuatiliaji na utoaji taarifa wa matumizi ya fedha za mikopo, urejeshaji wa fedha za mikopo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayolipwa na fedha za mikopo.

Mwongozo huu umetolewa leo tarehe 1 Mwezi Aprili, 2015.

Hawa A. Ghasia (Mb.)
WAZIRI WA NCHI
OWM - TAMISEMI

TAARIFA YA HALMASHAURI ZILIZOOMBA MIKOPO

MKOA	HALMASHAURI ILIYOKOPA	TAASISI YA FEDHA/ BENKI	TAREHE YA MKOPO	KIASI KILICHOKOPWA (SHS.)	RIBA	MUDA WA MKOPO	MADHUMUNI YA MKOPO	KIASI KILICHOREJESHWA (MKOPO + RIBA) (SHS.)


WM
WN
KM – OWM (T)
DLG
RAS
DED
KAMATI YA MRADI
BARAZA LA MADIWANI
KAMATI YA FEDHA
KAMATI YA FEDHA